



___ Maswali ya biblia ___

1.je ni nani mfalme gani aliye ingia katika hekalu la Mungu na kufukiza uvumba kama kuhani Mungu akampiga kwa ukoma?

2. Je. Amri ya tatu inasemaje?

3.je ni makosa gani ambayo daudi alimkosea Mungu hata,. Mungu akamwadhibu?

4.je wana wa Yusufu wakiume walikuwa wangapi na ni akina nani?

5. Maana ya Shalomu?

6.ni mifupa ya nani iliyo fufua mtu katika biblia?

8.je Bwana Yesu alifanya miujiza ya kuongeza samaki na mikate mara ngapi?

9.je stefano alikufa kwa kifo gani?

10.katika mitume wa Yesu (thenashara) ni wangapi vifo vyao vimerekodiwa katika biblia.

Bwana Yesu akubariki, shea na kwa wengine.



@NURU YA UPENDO

www.wingulamashahidi.org

0652274252 au 0693036618

07/02/2023

___MASAHIHISHO LEO___

MTIHANI WA BIBLIA (PART 19)

(Maswali ya biblia)

1. Je ni nani mfalme gani aliye ingia katika hekalu la Mungu na kufukiza uvumba kama kuhani Mungu akampiga kwa ukoma?

Jibu. MFALME UZIA

Soma. 2nyakati 26;16-23

2. Je. Amri ya tatu inasemaje?

Jibu. Kutoka 20:7

Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.

3. Je ni makosa gani ambayo daudi alimkosea Mungu hata,. Mungu akamwadhibu?

Jibu. 1)UZINZI NA KUUWA PASIPO HATIA

alizini na mke wa Uria kisha baadaye akamwua Uria katika vita

Soma. 2samweli 11:1-17



2)Aliwahesabu Israeli kwa kutaka kujitumainisha juu ya jeshi lake badala ya Mungu.

Soma. 1Nyakati 21;1-17

4.je wana wa Yusufu wakiume walikuwa wangapi na ni akina nani?

Jibu. Wawili

1)Manase

2)Efraimu

Soma. Mwanzo 41;50-52

5. Maana ya Shalomu?

Jibu. AMANI

Soma. Waamuzi 6;24

6.ni mifupa ya nani iliyo fufua mtu katika biblia?

Jibu. ELISHA

Soma. 2wafalme 13:20-21

8.je Bwana Yesu alifanya miujiza ya kuongeza samaki na mikate mara ngapi?

Jibu. MARA MBILI

1)Aliwalisha makutano kwa hesabu ya wanaume tuu 4000 (bila wanawake watoto kuhesabiwa) Kwa Mikate 7 na visamaki vichache

Soma. Malko 8;3-9

2)Aliwalisha makutano wanaume 5000 (bila hesabu ya wanawake na watoto) kwa mikate 5 na visamaki 2.

Soma. Yohana 6;8-10



9. je stefano alikufa kwa kifo gani?

Jibu. KWA KUPIGWA MAWE

Soma. Matendo ya mitume 7;54-60

10. katika mitume wa Yesu (thenashara) ni wangapi vifo vyao vimerekodiwa katika biblia.

Jibu. WAWILI

1) YUDA. Alijinyonga

soma Mathayo 27:3-5

2) YAKOBO. Alikatwa kichwa na Mfalme Helode.

soma matendo 13;1

Bwana Yesu akubariki, shea na kwa wengine.

@NURU YA UPENDO

www.wingulamashahidi.org

0652274252 au 0693036618